



# Uzalishaji bora wa mahindi



Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:  
Maruku Agricultural Research Institute, P.O.Box 127, Bukoba, Tanzania  
Tel:/Fax +255 732 983258;  
Email: marukuardi@yahoo.com

# Kutayarisha eneo



Ondoa miti, majani na magugu yote




Tifua eneo kwa kina kirefu



Sawazisha eneo vizuri ili kulaininisha udongo

# Kupanda



Panda mapema mara  
tu mvua inaponyesha

Chimba  
mashimo 75sm kati  
ya mistari na 60sm  
kati ya mashimo



# Mbolea ya kupandia



Weka aidha DAP au Minjingu mazao, au TSP kwa kila shimo (*angalia vipimo kwenye jedwali*)



Idadi ya vifuniko vya soda vilivyojaa kwa shimo

Aina ya Mbolea	Idadi ya gunia kwa ekari	Idadi ya vifuniko vya soda vilivyojaa kwa shimo
TSP/DAP	1	1½
Minjingu mazao	2	3
CAN (kama umeweke TSP)	2	3 (1½ wakati wa kupanda)

# Kutunza shamba



Panda mbegu  
kwenye mashimo  
ambayo mbegu  
hazikuota wiki 2  
baada ya kupanda



Palilia shamba mara  
tu magugu yanapoota  
baada ya hapo



Piga dawa ya kuuwa  
wadudu aina ya *stalk borer* (mf thiodan  
dust)

# Mbolea ya kukuzia



Chimba mashimo  
sm 5-10 katikati  
ya mimea 2, weka  
mbolea, kisha fukia  
kwa udongo



Weka mbolea ya  
kukuzia wiki 4-5  
baada ya mbegu  
kuota  
*(angalia vipimo  
kwenye jedwali)*

## Hakikisha mbolea haigusani na mimea moja kwa moja

Aina ya Mbolea	Idadi ya gunia kwa ekari	Idadi ya vifuniko vya soda vilivyoja kwa shimo
CAN	2	3 ( $1\frac{1}{2}$ wakati wa kukuzia)
Urea (kama uliweka Minjingu mazao)	2	3
Urea (kama uliweka DAP)	1	$1\frac{1}{2}$


# Kuvuna



Vuna mahindi mara tu mabua yanapokauka au mbegu za mahindi kuwa na mchirizi wa rangi nyeusi




Ondoa mahindi na magunzi yake kwenye maganda (usivune na maganda)



Weka mahindi kwenye turubai sio kwenye udongo

# Kukausha na kuhifadhi



- Anika mahindi kwenye turubai safi kwa siku 3-5
- Pukuchua mahindi kwa kupiga magunia kwa mti au pukuchua kwa mikono kama mahindi ni kwa ajili ya mbegu
- Pepeta mahindi kwa ungo
- Chambua mahindi ili kuondoa mahindi yaliyoharibika
- Changanya na dawa ya *Actellic super dust* ili kuzuia wadudu waharibifu wa mahindi wakati wa kuhifadhi
- Pakia mahindi kwenye magunia ya nailoni (magunia ya salfeti) halafu weka juu ya chanja ndani ya chumba kinachopitisha hewa vizuri lakini hakiruhusu mvua na jua kali kupita